East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 4, Issue 1, 2019
ISSN: 1476-4687

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Mchango wa Tamasha za Muziki Katika Ufundishaji wa Uainishaji wa Nyimbo Katika Shule za Upili Nchini Kenya

*Emilly Angushi Magambo[1]*, Dkt. Fred Simiyu[2] & Dkt. Deborah Amukowa[3]*

[1]Chuo Kikuu cha Kibabii, S.L.P 1699 – 50200, Bungoma, Kenya, emilymagambo77@gmail.com.
[2]Chuo Kikuu cha Kibabii, S.L.P 1699 – 50200, Bungoma, Kenya, wsimiyu@kibu.ac.ke.
[3]Chuo Kikuu cha Kibabii, S.L.P 1699 – 50200, Bungoma, Kenya, dnanyama@yahoo.com.

**Article history:**

*Received: 19 Aug 2019*
*Accepted: 21 Aug 2019*
*Published: 23 Aug 2019*

**Keywords**:

*Masimulizi,*
*Mchakato,*
*Msuko,*
*Matukio,*
*Wahusika,*
*Maudhui*

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza mchango wa tamasha za muziki katika ufundishaji na uainishaji wa nyimbo katika shule za upili nchini Kenya. Utafiti huu hasa ulilenga kupambanua uainishaji wa nyimbo katika tamasha za muziki, kudhihirisha namna uainishaji huu unavyoweza kutumiwa kufundishia uainishaji wa nyimbo darasani na kuonesha namna ambavyo uainishaji wa nyimbo katika tamasha za muziki huzisaidia nyimbo husika kutekeleza wajibu wake. Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu ufundishaji wa fasihi simulizi lakini kuna haja ya kuchunguza njia mbadala za ufundishaji wa kipera cha nyimbo kwa sababu ni kipana mno na hata uainishaji wake unakanganya. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya utanzu inayoonesha utaratibu wa kuainisha fasihi katika misingi ya aina mbalimbali kwa kuegemea miundo na maumbo, pamoja na nadharia ya ujifunzaji kijamii ambayo inashikilia kuwa ujifunzaji ni mchakato wa utambuzi ambao hujitokeza katika muktadha wa kijamii. Sampuli iliyolengwa katika utafiti huu ilijumuisha shule zilizoshiriki katika mashindano ya tamasha za muziki ya Kanda la Magharibi. Utafiti huu ulifanywa kwenye mashindano ya tamasha za muziki kiwango cha kikanda eneo la Magharibi yaliyofanyika katika shule ya upili ya wavulana ya Chavakali iliyo katika Kaunti ya Vihiga nchini Kenya. Kauli mbiu yake ilikuwa kuboresha umoja wa kitaifa kwa kuunganisha na kuleta watu pamoja. Watafitiwa ishirini na tano walihojiwa. Mbinu ya kuteua sampuli ilikuwa ya kinasibu na ya kimakusudi. Mtafiti alitumia utazamaji na mahojiano kama mbinu za kukusanya data. Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kutumia maelezo ya kiufafanuzi na kuwasilishwa kwa maandishi yaliyoambatana na mifano na picha. Mtafiti alipata kwamba nyimbo zimeainishwa katika madaraja mbalimbali kutegemea vigezo kama vile umri, mahali na maudhui. Utafiti huu ulibaini kuwa, tamasha za muziki zinaweza kuwa njia mbadala ya kufundishia uainishaji wa kipera cha nyimbo katika fasihi simulizi darasani. Umuhimu wa utafiti huu ni kuwa matokeo yake yataweza kuwafaidi wanafunzi na walimu katika ufundishaji wa nyimbo kama kipera cha fasihi simulizi.

## UTANGULIZI

Tamasha za muziki zimekuwepo kwa muda mrefu na kutumiwa kwa minajili ya kuwatuza washindi katika mashindano ya madaraja mbalimbali. Tamasha hizi huleta pamoja shule mbalimbali za msingi na upili. Tamasha hizi pia hutumiwa kuwaburudisha wengi wanaoshiriki kupitia madaraja maalum yanayowasilishwa, lakini utafiti huu ulilenga kudhihirisha namna madaraja haya yanavyoweza kutumiwa kufundishia kipera cha nyimbo hasa tukilenga uainishaji wake.

Kibiti (2018) alitafiti kuhusu matumizi ya tarakilishi katika ufundishaji wa fasihi simulizi na kubaini kuwa kuna changamoto zinazoathiri matumizi ya tarakilishi kama wenzo wa kufunzia. Beja (2000) alifanya utafiti kuhusu nyimbo za mbolezi za jamii ya Giriama, ambapo alipata kuwa nyimbo hizo zilisheheni umuhimu kadhaa kama vile kufariji waliofiwa na vilevile kuburudisha. Utafiti was Mutwiri (2005) kuhusu utendakazi wa nyiso katika jamii ya Watigania ulitambua kuwa nyiso zinaendelea kuimbwa katika jamii ya Watigania, sababu ikiwa majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na nyiso bado yako dhabiti. Utafiti wa Musembi (2016) nao kuhusu mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za jando kutoka jamii ya wakamba ulishadidia kuwa kadri hali ya maisha inavyoendelea kubadilika ndivyo nayo fasihi simulizi inavyobadilika. Gitonga (2017) alichunguza kuhusu uchambuzi linganishi wa fani na maudhui ya nyimbo za harusi za Kimeru na Kiswahili na kutambua kuwa kuna baadhi ya maudhui ambayo yanalingana katika nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili. Tafiti hizi zinalenga suala la ufundishaji na uainishaji wa nyimbo ila hazijashughulikia tamasha za muziki katika uainishaji wa nyimbo.

## MBINU ZA UTAFITI

### Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika shule ya upili ya wavulana ya Chavakali iliyopo katika Kaunti ya Vihiga nchini Kenya ambapo mashindano ya tamasha za muziki Kanda la Magharibi yalifanyika.

### Sampuli Lengwa

Sampuli lengwa katika utafiti huu ilikuwa ni wanafunzi na walimu walioshiriki katika tamasha za muziki Kanda la Magharibi mwaka 2018. Walliman (2011) anafafanua kuwa kundi lengwa ni jumla ya vitu vyote vinavyohusika katika kufanyiwa utafiti. Hivyo, nyimbo zilizowasilishwa katika tamasha za muziki zililengwa katika utafiti huu. Wanafunzi 20 na walimu 5 walihojiwa. Nyimbo 18 zilisanywa lakini 9 ziliteuliwa kutumika katika uchanganuzi.

### Usampulishaji

Sigh (2007) anashadidia kuwa usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Utafiti huu ulitumia usampulishaji nasibu katika kuteua wahojiwa. Ruane (2005) anafafanua kuwa usampulishaji nasibu ni mchakato wa kuchagua sampuli ambapo uwezekano wa kuchagua mshiriki yeyote katika kundi lengwa huwa kubwa. Vilevile usampulishaji wa kimakusudi ulitumiwa katika kuteua nyimbo zilizotumika katika utafiti huu. Hivi kwamba madaraja mahususi yalilengwa na mtafiti ili kupata data faafu.

### Mbinu za Kukusanya Data

Kothari (2004) anafafanua mbinu za ukusanyaji data kama jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Mtafiti alitumia mbinu za utazamaji, mahojiano na uchanganuzi wa yaliyomo ili kudhihirisha uainishaji wa nyimbo katika tamasha za muziki. Data iliyokusanywa ilihusu madaraja ya nyimbo zilizokusanywa kutoka tamasha za muziki. Mwongozo wa maswali ya mahojiano ya wanafunzi na walimu ilitumika, pamoja na ratiba ya utazamaji wa madaraja mahsusi ya tamasha za muziki. Data hii ilisanywa mwezi wa sita mwaka wa 2018.

### Uchanganuzi na uwasilishaji wa data

Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu kwa kuongozwa na mhimili wa pili wa nadharia ya utanzu inayoeleza kuwa tanzu huleta muwala katika matini na kufanya kazi ieleweke kwa urahisi sana, kupitia maelezo ya kiufafanuzi, huku mifano ya nyimbo husika

ikitolewa. Uwasilishaji wa data ulifanywa kwa kuzingatia malengo mahsusi ya utafiti huu. Data ya utafiti huu iliwasilishwa kwa kutumia maandishi yaliyoambatana na maelezo ya kiufafanuzi pamoja na picha, huku mifano ya nyimbo mahsusi ikitolewa.

## UCHANGANUZI WA DATA

### Uainishaji wa Nyimbo Katika Tamasha za Muziki Unavyoweza Kutumiwa Katika Kufundishia Uainishaji wa Nyimbo Darasani

Nyimbo katika tamasha za muziki zilikusanywa kwa kutumia nadharia ya ujifunzaji kijamiii mhimili wa tatu unaosema ujifunzaji hushirikisha utazamaji. Nyimbo hizi zilipatikana kupitia mbinu ya utazamaji na mahojiano. Nyimbo hizi zimechambuliwa kupitia maelezo ya kiufafanuzi kwa kutumia nadharia ya utanzu, mhimili wa pili unaoshadidia kuwa tanzu huleta muwala katika matini na kufanya kazi ieleweke kwa urahisi sana. Kwa mujibu wa Mulokozi (1996) kuna nyimbo za kazi, za harusi, jando na unyago, ibada na matambiko, maombolezi na nyinginezo. Wanjala (2013) anahoji kuwa nyimbo zinaweza kugawanywa katika aina mbalimbali kama vile nyimbo za siasa, nyimbo za kazi na nyimbo za matanga. Kulingana na Wamitilla (2003) kuna aina zifuatazo za nyimbo; bembelezi, nyimbo za watoto, wawe, kimai, mbolezi, nyimbo za kisiasa, nyimbo za kazi, tenzi, tumbuizo na jadiya. Ngure (2003) anatambua aina kumi na mbili za nyimbo, mathalan, nyimbo za kazi, vita, tohara, harusi, nyimbo za kuzaliwa na kupatiwa jina mtoto, kafara, mapenzi, matanga, kilio, mazishi na za sifa. Tamasha za muziki zimezua uainishaji ufuatao mpya wa nyimbo ambao waweza kusaidia kufunzia aina zilizopo.

### *Uainishaji wa Kiumri*

Katika tamasha za muziki, nyimbo za watoto ziliimbwa na watoto wa shule za chekechea na shule za msingi. Nyimbo hizi ziliimbwa chini ya daraja 801H la watoto wa shule za msingi na 801G la shule za chekechea. ‘H’ ilisimamia shule za msingi huku ‘G’ ikisimamia shule za chekechea. Nyimbo hizo zilikuwa za kutoka nchi za ughaibuni pamoja na za kutoka Bara la Afrika. Vigezo vilivyotiliwa maanani katika uainishaji huu ni umri wa watoto, kwamba watoto walioimba nyimbo hizi walistahili wawe wa shule za chekechea na wa darasa la kwanza hadi la tatu. Jambo linaloshadidiwa na Wamitila (k.h.j) kwamba nyimbo za watoto huimbwa wakati wa michezo yao na huandamana na vitendo kama kuruka na kugusia vitu vinavyopatikana katika mazingira ya jamii husika. Wakaguzi waliweza kuzingatia uimbaji na maleba ya watoto hawa. Iwapo nyimbo zao zilihusu nchi za ng’ambo mavazi yao yaliandamana na hizo nyimbo. Zile zilizohusu Bara la Afrika ziliambatana na maleba yaliyosheheni sehemu ambapo wimbo huo ulitolewa.

Darasani wanafunzi hufunzwa kigezo cha umri tu katika uainishaji huu kwa ujumla, kwamba hizo ni nyimbo za watoto. Tamasha za muziki zilikuwa na uanishaji mpana kwa mfano mbali na kuzingatia umri, walizingatia pia maleba na sehemu ambapo wimbo huo uligusia, wataalamu kama vile Wamitila (k.h.j) wameainisha hizi nyimbo kama nyimbo za watoto, ila katika tamasha za muziki, mbali na kuwa ni nyimbo za watoto, ziliainishwa kulingana na kigezo cha mahali na idadi ya wahusika kwa mfano daraja 100 lilishirikisha mwimbaji mmoja wa miaka 3 hadi 5 na kuzua uainishaji mseto. Ifuatayo ni sehemu ya mfano wa wimbo wa watoto kutoka nchi za ughaibuni uliowasilishwa katika tamasha za muziki 2018 chini ya daraja 801H linalohusisha shule za msingi darasa la 1 hadi 3. Wimbo “*follow my house to London town*” ulihusisha watoto wa shule za msingi wakiimba na kucheza.

*Asubuhi na mapema,*
*Nikienda kule London,*
*Wakati wa London, wakati wa London,*
*Mapema sana asubuhi,*
*Mpaka jioni na rafiki zangu,*
*Wakati tunapocheza,*
*Tunacheza na kamba,*
*Tunacheza na mpira*,
*Siku ya Jumapili*.



***Picha 1: Watoto wa shule ya chekechea wakiimba***

***Uainishaji wa Kimaudhui***

Katika uainishaji huu kulikuwa na nyimbo za kazi, mtafiti alitambua kuwa ziliweza kuainishwa tofauti kupitia madaraja mahsusi. Kwa mfano kupitia daraja 365 kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

*Tuyafyeke haya magugu, tuyafyeke,*
*Kwa miundu tuyafyeke, tuyafyeke*
*Kwa pamoja tuyafyekeeee,*
*Kwa nguvu tuyafyekeeee.*


Hata hivyo uainishaji mwingine wa nyimbo za kazi ulibainika katika nyimbo zilizohusu huduma tofauti kwa umma kupitia daraja 361. Utafiti huu ukabaini kuwa tamasha za muziki zingeweza kuwa nyenzo nyingine ya kufundishia nyimbo za kazi. Hivyo tamasha za muziki zikawa dhihirisho tosha kwamba zinaweza kutumiwa kama mbinu mbadala ya kufundishia aina hii ya nyimbo darasani. Jambo hili lilishadidiwa na watafitiwa walipokuwa wakihojiwa na mtafiti kwamba nyimbo za kazi zinazofundishwa darasani huweza kudhihirika katika utendaji zinapowasilishwa katika tamasha za muziki.



***Picha 2: Wanafunzi wa shule ya msingi wakijitayarisha kuimba wimbo wa kazi***

Kwenye tamasha za muziki madaraja tofauti yalisheheni nyimbo za maudhui ya mapenzi kwa mfano daraja 391 na 392. Daraja 391 lilijumuisha nyimbo "zilizopendwa" kutoka nchi ya Kenya, ilhali daraja 392 likasheheni nyimbo "zilizopendwa" kutoka nchi nyingine barani Afrika. Nyimbo hizi darasani huitwa nyimbo za mapenzi kulingana na wataalamu kama vile Ngure (k.h.j) ila katika tamasha za muziki ziliitwa nyimbo "zilizopendwa", lakini zilisheheni vilevile maudhui ya mapenzi na kilio. Nyimbo hizi pia zilishuhudiwa katika daraja 346 ambalo lilihusu nyimbo za taarab ambapo nyingi za nyimbo hizo zilihusu mapenzi. Wahojiwa walikiri kuwa wanafunzi darasani wanawezafaidika zaidi kutokana na kutazama nyimbo hizi iwapo zitahifadhiwa kwenye kanda za video na kutumiwa darasani. Jambo hili litawezesha kuelewa zaidi uainishaji wa nyimbo katika fasihi simulizi, mfano wa wimbo wa mapenzi na kilio ulipatikana katika sehemu ya wimbo "Susana" ulioimbwa kupitia daraja 391.

*Nakulia oh Susana,*
*Nakulia oh Susana!*
*Nakulia wewe Susana.*
*Nakulia mama Susana*
*Nakulia, nakulia, nakulia oh Susana.*



***Picha 3: Wanafunzi wa shule ya upili wakiwasilisha wimbo wa mapenzi***

Kwenye tamasha za muziki nyimbo za kumsifu Mungu ziliwasilishwa chini ya daraja 322 ambalo lilihusu nyimbo za dini ya Kikristo na 341 zilizosheheni nyimbo za dini ya Kislamu. Darasani nyimbo hizi hufunzwa kama kipengele kimoja cha nyimbo za dini kulingana na wataalamu kama ilivyoshuhudiwa hapo juu, ila kwenye tamasha za muziki uainishaji zaidi umefanywa na kuzitenga katika madaraja yao mahususi ya nyimbo za Kikristo na nyimbo za Kiislamu na kudhirishwa zaidi kuwa nyimbo za dini kupitia mavazi au maleba na vifaa au vyombo vilivyotumika. Hivyo basi tamasha za muziki kuwa na mchango zaidi katika uainishaji wa nyimbo darasani, mfano wa sehemu ya wimbo wa dini ya kikristo chini ya daraja 322.

*Ninaona! Ninaona!*
*Bwana Yesu ameketi kitini mawinguni,*
*Ninaona! Ninaona!*
*Bwana Yesu ameketi kitini mawinguni,*
*Roho atakuja, roho,*
*Roho atakuja, roho anaishi*
*Haleluhya.*



***Picha 4: Wanafunzi wa shule ya upili wakijiandaa kuwasilisha wimbo wa dini ya kikristo***

Katika tamasha za muziki kulikuwa na nyimbo za maudhui ya sifa chini ya daraja 261. Uainishaji huu ulibainika kupitia nyimbo zilizoimbwa kumiminia sifa watu au makundi mbalimbali kwa mchango wao katika jamii. Nyimbo hizi ziliimbwa chini ya utunzi maalum kama vile kuendeleza huduma kwa umma. Mfano wanafunzi wa shule za msingi waliimba wimbo ufuatao kusifu mwalimu wao, kwamba bila mwalimu hawangeweza lolote.

*Hapa shuleni kielimu mengi tunayapokea,*
*Ila pasipo mwalimu katu tusingeyaweza,*
*Ila pasipo mwalimu katu tusingeyaweza.*



***Picha 5: Wanafunzi wa shule ya msingi wakiwasilisha wimbo wa sifa***

Mtafiti alishuhudia nyimbo za maudhui ya kuomboleza kupitia utazamaji zikiimbwa katika madaraja mbalimbali ya nyimbo za jadiya na hivyo tamasha za muziki kuwa na mchango katika uainishaji wa nyimbo hizi darasani. Jambo hili laweza kutekelezwa kupitia video zilizonaswa kwenye tamasha za muziki, mfano wa mbolezi ulipatikana katika daraja 371 (Mushere wanje –mke wangu).

*Ninalia nikifikiria koo! Mke wangu,*
*Ninalia nikifikiria koo! Mke wangu,*
*Mke wangu ndiye alikuwa akinipikia ugali,*
*Lakini siku hizi ugali ni mbichi!*

Katika tamasha za muziki wahojiwa walikiri kushiriki katika daraja lililoshughulikia nyimbo za mbolezi, ila hazikuitwa hivyo kwa vile nyingine zilipatikana katika madaraja yaliyoshirikisha nyimbo za jadiya na kuzua suala la ugilgili katika fasihi simulizi ambapo tanzu huweza kuingiliana na kuzua uainishaji mseto.



***Picha 6: Wanafunzi wa shule ya upili wakiwasilisha wimbo wa mbolezi***

Nyimbo zenye maudhui ya tohara zilitokea katika nyimbo za jadiya kutoka makabila mbalimbali kwa vile hapakuwa na daraja mahususi la aina hizi za nyimbo na kuzua ufaraguzi ambao ndio unaoweza kusaidia sana katika ufindishaji wa nyimbo darasani. Nyimbo hizi hazijafungwa tu katika uainishaji mmoja, kwa hivyo tamasha za muziki zikawa chungu kuu la kusaidia walimu katika ufundishaji wa kipera cha nyimbo darasani kwa matumizi ya mifano iliyohifadhiwa katika kanda za video. Wimbo ufuatao ni sehemu ya mfano wa nyiso, ambao ulipatikana chini ya daraja 373 kutoka jamii ya asabaot (Choolieet- tohara).

*Ulisema,*
*Tohara, sherehe ya tohara eeh!*
*Sherehe yangu ya tohara ni nzuri,*
*Ndio sherehe ya tohara ni yetu,*
*Ulisema tohara, sherehe ya tohara eeh!*
*Wavulana kama hawa ni wazuri.*

Uwasilishaji wa nyiso katika tamasha ni hai na huzingatia pia maleba kulingana na jamii inayohusika.



***Picha 7: Wanafunzi wa shule ya upili wakiwasilisha wimbo wa nyiso***

Katika tamasha za muziki nyimbo za maudhui ya harusi ziliimbwa kupitia nyimbo za jadiya na hata kupitia daraja la taarab la 346. Mtafiti alishuhudia uwasilishaji wa nyimbo hizi kupitia utazamaji. Tamasha za muziki zikadhirika kuwa na mchango katika ufundishaji wa nyimbo hizi kwa mfano wimbo wa Kisabaot wa daraja 373 ufuatao (Araap Mbaanya- mtoto wa mbaanya) mstari wa tatu unaosema kuunganisha wana ndoa:

*Mtoto wa mbaanyaa ndio kweli mtoto wa mbaanyaa,*
*Asiye na roho mbaya, mtoto wa mbaanyaa twataka watoto,*
*Kuuunganisha wanandoa, ndio,*
*Kuunganisha wanandoa, ndio,*
*Huu ni wimbo unaoimbwa katika jamii ya wasabaot ili kuunganisha wanandoa*.



***Picha 8: Wanafunzi wa shule ya upili wakiwasilisha wimbo wa harusi***

***Uainishaji wa Mahali***

Nyimbo hizi ziliimbwa kupitia madaraja tofauti tofauti yaliyosheheni nyimbo kutoka tamaduni mahususi. Uainishaji wa nyimbo hizi katika tamasha za muziki ulilenga maeneo mbali mbali na zinavyofunzwa darasani, kwa mfano daaraja 371 lilitengewa nyimbo kutoka Ujaluoni na kutoka maeneo ya Waluhya; 372 sehemu za Kisii; 374 Turkana; 375 Somali na 379 Teso.

***Uainishaji wa Kijinsia***

Nyimbo za watoto ziliainishwa kulingana na jinsia, kwa mfano daraja 202 lilihusu nyimbo zilizoimbwa na wasichana pekee na 212 zikaimbwa na wavulana pekee. Walipoimba pamoja uainishaji ulibadilika na kuwa 222. Haya madaraja 202, 212 na 222 yalihusu nyimbo za kujichagulia za kidini. Lakini walipojitungia nyimbo zao uainishaji ulibadilika na

kuwa 203 kwa wasichana, 213 kwa wavulana na 223 wakiimba pamoja.

***Uainishaji wa Kiidadi***

Tamasha za muziki ziliainisha nyimbo kulingana na idadi ya wahusika. Kwa mfano kwaya ndogo zilistahili kuwa na washiriki kati ya 8 na 16, kwaya wastani washiriki 30 hadi 42 na kwaya kubwa washiriki 48 hadi 60. Mifano ya madaraja yalikuwa 203 ya shule za msingi na 303 shule za upili nyimbo za kujitungia za dini.

## HITIMISHO

Katika makala hii tumedhihirisha namna uainishaji wa nyimbo katika tamasha za muziki unavyoweza kutumiwa kufundishia uainishaji wa nyimbo darasani, hivyo kuzua mbinu mbadala ya kufundishia uainishaji wa nyimbo. Nyimbo katika tamasha za muziki zikihifadhiwa kwenye kanda za video zinaweza kuwa na mchango katika ufundishaji wa uainishaji wa nyimbo darasani. Fasihi simulizi ni hai na kwa hivyo haitakuwa kamilifu bila kutazamwa uhai wake, ambapo tamasha za muziki zinachangia kuendeleza swala hili la uhai wa fasihi, katika kushiriki tamasha za muziki na kupitia kanda za video za tamasha za muziki zilizohifadhiwa wanafunzi wataelewa vyema uainishaji wa nyimbo wanapofundishwa darasani. Isitoshe tamasha za muziki zimedhihirishwa kuwa na uainishaji wa hali ya juu wa nyimbo kuliko walivyofanya wataalamu tofauti tofauti. Utafiti huu umeonesha kwamba vigezo vilivyotumiwa kuainisha nyimbo na kuziweka katika madaraja tofauti katika tamasha za muziki ni vingi mno kuliko vile vilivyotumiwa na wataalamu walioainisha nyimbo hapo awali, hivyo kuboresha uainishaji wa nyimbo. Utafiti huu unapendekeza kwamba tamasha za muziki zitumiwe kufundishia uanishaji wa nyimbo darasani. Tamasha hizi zichukuliwe kama mojawapo wa nyenzo za kufundishia fasihi simulizi.

## MAREJELEO


Beja, S.K. (2000). *Giriama Funeral Songs. A functional Aesthetic Study*. Tasnifu ya uzamifu chuo kikuu cha Nairobi.

Gitonga, N. W. (2017). *Uchambuzi linganishi wa Fani na maudhi ya nyimbo za harusi za Kimeru na za Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu za Nairobi.

Kibiti, D.B. (2018). *Matumizi ya tarakilishikatikamufundishsji wa fasihi simulizi katika shule za upili nchini Kenya.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Kibabii.

Kothari, C.R. (2004). *Research Methodology. Methods and Techniques.* (Toleo la 2) New Delhi: New Age International (P) Limited.

Mulokozi, M.M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili.* Dar es Salam. TUKI.

Musembi, N.N (2006). *Mabadiliko ya maudhui katika nyimbo za jando, mfano kutoka jamii ya Kamba.* Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Mt. Kenya.

Mutwiri, G. (2005). *Mitazamo ya utendakazi wa nyiso katika jamii ya Watigana*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Ngure, A. (2003), *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari.* Nairobi. Phoenix Publishers.

Ruane, J.M. (2005. *Essentials of Research Methods. Aguide to Social Sciences Research*. Australia; Blackwell Publishing.

Sigh, K. (2007). *Quantitative Social Research Methods*. India: SAG Publication.

Wallman, N. (2011). *Research Methods: The Basic.* London & New York: Routeledge Taylor of Francos Group.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wanjala, F.S. (2013). *Kitovu cha Fasihi Simulizi kwa Shule*, Vyuo na Ndaki Mwanza; Serenget Educational Publishers (T) Ltd.